Wananchi hatarini kukabiliwa na njaa [Send to a friend]

Monday, 12 March 2012 09:44

Anthony Mayunga,Bunda
WAKAZI wa Kijiji cha Migungani, Kata ya Migungani katika mamlaka ya mji mdogo wa Bunda, wanakabiliwa na tishio la njaa baada ya mazao ya mpunga kuathiriwa na maji yanayodaiwa kuwa na sumu yaliyotiririshwa na kiwanda cha Bundaa Oil Mill.

Kukauka kwa mazao hayo ambayo wanategemea kwa biashara na chakula kumesababisha baadhi ya wananchi kuomba serikali kuandaa utaratibu wa kuwapatia chakula cha msaada.

Uchunguzi wa Mwananchi katika mashamba ya wananchi, umebaini kuwa mazao yote yaliyoingiwa na maji ya sumu, Novemba 6, mwaka 2011 yameungua na wakulima hawakuweza kuvuna chochote.

Pia madhara ya maji hayo yanaonekana kuwa makubwa zaidi kwa kuharibu ardhi hiyo ambayo wanayoitegemea kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

Maswi Chogo mmoja wa waathirika na maji hayo alisema ana ekari tano za mpunga ambazo, ziliaharibiwa na maji hayo na kufidiwa Sh25,000 za kununua mbegu.

“Unanunua mbegu kupanda wapi maana ekari hizo nilitegemea kupata zaidi ya magunia 100 ya mpunga sasa unapewa hela ya kununua debe moja upande kwenye ardhi ambayo imeharibiika,serikali inahusika kutuhujumu
sisi kwa kushirikiana na mwekezaji kweli?”alihoji kwa ukali akiwa shambani kwake.

Alisema wao wanatembea wamekufa kwa kuwa maji ya kunywa,kuoga, mifugo na mazao wanayokula yamekuwa yakichafuliwa na maji ya sumu ambayo hutiririshwa.

Kichere Gikaro alisema zaidi ya ekari 55 zilichafuliwa na maji hayo mwishoni mwa mwaka jana, lakini alipewa Sh1 milioni kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa kata hiyo na kwamba fedha zilizowafikia wakazi 25 kwa ajili ya kununua mbegu ni Sh875,000.

Uchunguzi zaidi wa Mwananchi umebaini bei ya mchele katika soko la Bunda imepanda kutoka Sh 1,800 mpaka Sh2,300 kwa kilo moja tofauti Wilaya ya Serengeti ambako kilo moja inauzwa Sh2,000.

**Halmashauri yatoa notisi.**
Kutokana na kampuni hiyo kukaidi maagizo yanayotolewa na serikali
halmashauri ya wilaya hiyo imetoa notisi ya siku 30 ikitishia kufunga kiwanda na kuwafikisha mahakamani uongozi kwa kukiuka sheria ya mazingira Na 20/2004.

Barua iliyosainiwa na Ofisa Mazingira wa Wilaya Stafa Nashon kwaniaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo inabainisha kuwa uongozi wa kiwanda hicho unakaidi maagizo yanayotolewa na watalaamu wa mazingira na kuendelea kutiririsha maji ya sumu kwa jamii.

"Katika ukaguzi wa januari 26,2012 ilibainika pamoja na maelekezo yaliyotolewa kufuatia ukaguzi uliofanyika siku za nyuma bado kuna maji yanazidi kutiririka kwenda katika mashamba yaliyoko jirani," ilibainisha taarifa.

Pia kampuni ilipuuza agizo la kuitaka ivute maji ya sumu yaliyoko kwenye bwawa la kutunzia maji kutoka kiwandani ili yarudishwe kwenye mtambo wa kuchujia, lakini haikufanya hivyo.

Afisa mazingira amebainisha kuwa kiwanda hicho kinatumia kiasi kikubwa cha miti kama chanzo cha nishati wakati hakina hata msitu waliowahi kupanda.

"Wafanyakazi wa kiwanda kwa kiasi kikubwa hawana vifaa vya kinga kama viatu, ovaroli, kofia na miwani, tena kiwanda hakina mtaalamu wa maabara kwa wakati wote wa uzalishaji,"alisisitiza kwenye notisi hiyo.

**Mkurugenzi wa kiwanda acharuka**
Mkurugenzi wa kiwanda hicho Rajesh Savla alipoulizwa na Mwananchi kuhusu kukataa kutekeleza matakwa ya uongozi wa halmashauri hiyo aliasema: "Weye uliza watu wa Mazingira, mimi sina matatizo naendelea na kazi kama kawaida,mbona wewe unafuatilia sana hii maneno.

Alipotakiwa kutoa ufafanuzi anaendeleaje na kazi za uzalishaji wakati hana mtaalamu wa maabara na mtambo wa kuchuja maji machafu haufanyi kazi alisema: "Nani anakwambia mambo yote ya kiwandani kwangu. Baada ya kusema hivyo alikata simu.

**Wanaharakati wa mazingira.**
Stanslaus Nyembea kutoka chama cha wanasheria wa Mazingira (Lawyers' Environmental Action Team (LEATt) alisema pamoja na hatua zilizokwisha fikiwa na halmashauri, lakini wanafikiri kuchukua hatua za kisheria kwa niaba ya wananchi waliokwisha pata madhara.

**Naye Salinge ambaye ni wakili kutoka shirika la Pastoralist Indigenous**

None Government Organisation Forum (Pingo's) linalojihusisha na utetezi wa jamii ya wafugaji na warina asali alisema wameishaanza hatua za awali kuhakikisha wanawatetea wananchi kutokana na mifugo yao mingi kufa ili waweze kulipwa.